**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

**KAMATI YA KUDUMU YA BAJETI**

# MAONI YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MFUKO WA BUNGE KWA MWAKA WA FEDHA 2019/20 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21

**DODOMA**

**APRILI, 2020**

**YALIYOMO**

1.0. UTANGULIZI ........................................................................................................ 1

2.0. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2019/20 ............ 2

2.1 Matumizi ya Kawaida ........................................................................................ 3

2.2 Matumizi ya Fedha za Maendeleo .................................................................. 3

2.3 Maduhuli ............................................................................................................ 4

3.0 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA MFUKO WA BUNGE KWA MWAKA WA FEDHA 2019/20 ........................................................................................................ 4

4.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA MFUKO WA BUNGE KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21 ........................................................................................ 7

4.1 Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2020/21 ........................ 7

4.2 Shughuli zitakazotekelezwa Katika Mwaka wa Fedha 2020/21 ................. 7

5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI ...................................................................... 10

6.0 HITIMISHO. ........................................................................................................ 11

## MAONI YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MFUKO WA BUNGE KWA MWAKA WA FEDHA 2019/20 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21

## 1.0. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bajeti, kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2019/20 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2020/21.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa kifungu cha 71 (b) cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015, kamati ilikutana na Mheshimiwa Dkt. Philip Isidor Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Jenista Joackim Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, kazi, Vijana, Ajira na Walemavu) pamoja na Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai na kupitia utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2019/20 pamoja na kufanya mashauriano kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2020/21.

**Mheshimiwa Spika,** taarifa hii inatoa mrejesho kwa Bunge lako Tukufu kuhusu utekelezaji wa bajeti na majukumu ya Mfuko wa Bunge hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2020, pamoja na vipaumbele na masuala muhimu yanayopendekezwa katika Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2020/2021.

## 2.0. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

**Mheshimiwa Spika,** katika kuwezesha Ofisi ya Bunge kutekeleza majukumu yake, Kifungu cha 32 cha Sheria ya Uendeshaji wa Bunge kama ilivyofanyiwa rejea mwaka 2015 kilianzisha Mfuko wa Bunge. Hivyo, Mfuko wa Bunge hutengewa fedha kwa ajili ya kugharamia mahitaji mbalimbali, ambapo **asilimia 85** ya mahitaji hayo ya fedha hutumika kugharamia Mikutano ya Bunge, Kamati za Bunge, posho ya Jimbo na usafiri kwa Wabunge, matibabu kwa Wabunge na sehemu iliyobaki **asilimia 15** hutumika kutekeleza shughuli za utawala na uendeshaji.

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Bunge inatekeleza Bajeti yake kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti, Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma pamoja na Mpango Mkakati wa Ofisi ya Bunge (*Strategic Plan 2016-2021*) na Mpango wa Muda wa Kati (*Medium Term Expenditure Framework)*. Utekelezaji wa Bajeti umezingitia malengo yaliyotarajiwa kutekelezwa katika vipindi husika na makisio ya Bajeti yamezingatia kuboresha na kutoa huduma mbali mbali kulingana na mahitaji halisi.

### 2.1. Bajeti ya Mfuko wa Bunge iliyoidhinishwa kwa mwaka 2019/20

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2019/20 Mfuko wa Bunge – Fungu 42 uliidhinishiwa jumla ya kiasi cha **Sh.124,182,537,600.00.** Kati ya fedha hizo **Sh.23,334,462,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara (PE), **Sh.93,238,564,000.00** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na **Sh.7,609,511,600.00** kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo. Kati ya fedha za Maendeleo **Sh.5,000,000,000.00** ni fedha za ndani na **Sh.2,609,511,600.00** ni

fedha za Nje. Vilevile, Mfuko wa Bunge uliidhinishiwa kukusanya maduhuli ya kiasi cha **Sh.54, 777,000. 00.**

## 2.2. Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia 15 Machi, 2020 Mfuko wa Bunge ulikuwa umepokea fedha za matumizi ya kawaida kiasi cha **Sh.77,609,331,502.** Kati ya fedha hizo **Sh. Sh.62,080,604,202** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) sawa na **asilimia 66.6** ya bajeti yote na **Sh. 15,121,576,780** kwa ajili ya mishahara (PE) sawa na **asilimia 66.5.**

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla utolewaji wa fedha za matumizi ya kawaida (mishahara na OC) umekuwa mzuri na umewezesha Ofisi ya Bunge na Bunge lako Tukufu kutekeleza majukumu yake vizuri.

## 2.2 Matumizi ya Fedha za Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2020 kiasi cha **Sh. 5,233,746,339.35** sawa na **asilimia 69** ya fedha zote za maendeleo zilizotengwa kwa mwaka 2019/2020 zilikuwa zimepokelewa kwa ajili ya kutekeleza shughuli zilizopangwa ambazo ni sawa na **asilimia 68.8**. fedha hizo zilipangwa kutekeleza miradi minne ikiwa ni pamoja na ukarabati wa Majengo ya Bunge, Ujenzi wa Miundombinu ya Bunge, Mradi wa kujengea uwezo Wabunge na Watumishi (LSP) pamoja na Mradi wa Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP).

## 2.3 Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2019/20 Mfuko wa Bunge uliidhinishiwa kukusanya maduhuli ya **Sh. 54, 777,000. 00**, hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2020 kiasi cha **Sh.49,404,550.78** sawa na **asilimia 90.2** kimekusanywa. Makusanyo ya maduhuli haya yametokana na kodi ya pango, marejesho ya masurufu pamoja na kuuza nyaraka za zabuni.

# 3.0 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA MFUKO WA BUNGE KWA MWAKA WA FEDHA 2019/20.

## 3.1 Utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Bunge

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua fursa hii kuipongeza Ofisi ya Bunge kwa kutekeleza vyema malengo yake kwa mwaka uliotangulia ikiwa ni pamoja na mipango mizuri waliyojiwekea kwa mwaka huu wa Fedha.

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai, 2019 hadi tarehe 15 Machi, 2020 Mfuko wa Bunge (Fungu – 42) umefanikisha kutekeleza shughuli mbalimbali ukiwemo uratibu wa shughuli za Bunge kama ifuatavyo:-

i) Kuimarisha utendaji wa Bunge kwa kutumia mfumo wa Bunge Mtandao (*e-Parliament*) na hivyo kuongeza ufanisi wa Bunge katika kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali;
ii) Kuratibu na kusimamia shughuli za Mikutano Mitatu ya Bunge (16,17 na 18) na Mikutano Mitatu ya Kamati;
iii) Kutoa ushauri wa Kisheria kwa Wabunge na uchambuzi wa Miswada;

iv) Kuratibu, kuchapisha na kutunza Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard) pamoja na nyaraka mbalimbali za Bunge na Serikali;

v) Kugharamia malipo ya stahili za Wabunge (Posho ya Jimbo na usafiri) pamoja na matibabu ya Wabunge na familia zao;

vi) Kuratibu shughuli za Ofisi za Viongozi, Tume ya Utumishi wa Bunge na Utawala;

vii) Kutoa huduma mbalimbali za Utafiti kwa Wabunge zinazohusiana na masuala ya kiuchumi, kisiasa na kijamii;

viii) Kutolewa kwa mafunzo mbalimbali kwa Wabunge na Watumishi;

ix) Kuratibu stahili za Watumishi;

x) Kuwezesha ushiriki wa Bunge katika Mikutano ya Kimataifa ambayo Bunge ni mwanachama ambayo ni SADC PF, PAP, CPA, Great Lakes, IPU, ACP-EU;

xi) Kuwezesha Wabunge kushiriki mashindano ya michezo kwa Mabunge ya Jumuiya ya Afrika mashariki;

xii) Kuratibu kazi ya utoaji wa habari kwa wananchi kuhusu shughuli za Kamati na Bunge pamoja na kutoa elimu kwa umma kwa wadau na wageni waliotembelea Bunge;

xiii) Kuandaa vipindi vya Televisheni na kurusha matangazo ya Bunge;

xiv) Ukarabati wa Majengo ya Ofisi pamoja na Ujenzi wa Makazi ya Viongozi ambapo hadi kufikia tarehe 15 Machi 2020, Mfuko wa Bunge (Fungu – 42) umeweza kusimamia na kuratibu kazi zifuatazo:-

- Uboreshaji wa Majengo ya Ofisi.
- Uboreshaji wa Ukumbi wa Bunge.
- Ujenzi wa Nyumba za Viongozi.

xv) Usimamizi wa matumizi ya fedha zilizokasimiwa kwenye Mfuko wa Bunge ulifanyika kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti, Sheria ya Fedha za Umma na Sheria ya Manunuzi ya Umma; na

## 3.2 Mafanikio ya Utekelezaji

**Mheshimiwa Spika**, Mfuko wa Bunge umeweza kufanikisha yafuatayo:-

a) Kutekeleza shughuli za Bunge kwa kutumia TEHAMA kupitia mfumo wa Bunge Mtandao *(e-Parliament)* uliotengenezwa na kusimamiwa na wataalamu wa ndani wa Ofisi ya Bunge wakisaidiana na Wataalamu wa e-Government (e-Ga). Kwa, sasa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali zinawasilisha taarifa na nyaraka mbalimbali Bungeni kwa kutumia nakala tete *(Softcopy)* badala ya nakala ngumu *(Hard copy)* kama ilivyokuwa awali. Hatua hii imeweza kupunguza gharama za uendeshaji na hivyo kuokoa shilingi bilioni 2 kwa upande wa Bunge kilichotarajiwa kutumika kuanzia Mwezi Novemba 2019 hadi Juni 2020 katika uandaaji na uhifadhi wa nyaraka mbalimbali zinazoandaliwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Bunge. Aidha, kupitia mfumo huu inakadiriwa kuwa, kwa kipindi cha Mwaka mzima, Serikali inaweza kuokoa kiasi cha zaidi shilingi bilioni 100.

b) Kuzinduliwa kwa '*Bunge Mobile Application*' unaowezesha Waheshimiwa Wabunge pamoja na wadau mbalimbali kupata taarifa mbalimbali za shughuli za Bunge kupitia simu za mkononi kama vile orodha ya shughuli za Bunge (order paper), *hansard* pamoja na sheria na miswada iliyopitishwa na Bunge;

c) Kuboresha kwa muonekano wa picha na urushaji wa matangazo kupitia Bunge studio kwa kununua vifaa vipya na vya kisasa vya studio hiyo;

d) Kupandishwa vyeo kwa watumishi arobaini na tano (45) na kuwabadilisha kada watumishi nane (8);

e) Kuimarisha ulinzi na usalama katika maeneo ya Bunge, kwa Wabunge, watumishi na wageni mbalimbali wanaoingia kwenye maeneo ya Bunge ikiwa ni pamoja na kununua vifaa vipya vya ulinzi na usalama;

f) Mfuko wa Bunge umekuwa ukipokea fedha kulingana na Mpango Kazi na maombi yanayowasilishwa Hazina na hivyo kuweza kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

g) Kushiriki kwenye Michezo ya Kumi (10) ya Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyofanyika nchini Uganda Mwezi Disemba 2019. Timu ya Bunge la Tanzania ilipata ushindi wa pili wa Jumla na kupata Medali za Dhahabu Tano (5), Medali za Fedha Kumi (10) na Medali za Shaba Tatu (3) kwa michezo yote iliyoshiriki.

## 4.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA MFUKO WA BUNGE KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21

### 4.1 Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2020/21

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** katika mwaka wa fedha 2020/21 Mfuko wa Bunge unaomba kutengewa jumla ya **Sh. 121,786,257,000.** Kati ya kiasi hicho, **Sh. 23,253,494,000.00** zimepangwa kwa ajili ya Mishahara ya Wabunge na Watumishi, **Sh. 90,314,153,000.00** zimepangwa kwa ajili ya matumizi mengineyo na **Sh**. **8,218,610,000.00** zinaombwa katika Mpango wa Maendeleo ambapo **Sh. 5,000,000,000.00** ni fedha za ndani na **Sh. 3,218,610,000.00** ni fedha za nje. Aidha, hadi kufikia Juni 30, 2021 Ofisi imepanga kukusanya maduhuli yenye jumla ya **Sh. 76,215,500.**

**Mheshimiwa Spika,** maombi haya ya fedha kwa mwaka wa fedha 2020/21 yamezingatia mahitaji ya msingi yakiwemo mahitaji ya shughuli za Bunge (Mikutano ya Bunge na Kamati za Bunge) na uendeshaji wa Ofisi. Hivyo, Mfuko wa Bunge umepanga kutekeleza shughuli za vipaumbele kama ifuatavyo: -

a) Kuratibu na kusimamia shughuli za Mkutano wa Bajeti (1) na Mikutano Midogo Miwili (2) ya Bunge;
b) Kuratibu na kusimamia shughuli za Mikutano mitatu (3) ya Kamati za Kudumu za Bunge ambayo ni Mkutano Mmoja wa Kamati kuhusu uchambuzi wa bajeti na Mikutano Midogo Miwili (2);
c) Kuwezesha shughuli za Wabunge katika majimbo na maeneo yao ya uwakilishi;
d) Kuratibu na kuchapisha Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*) pamoja na nyaraka mbalimbali za Bunge na Serikali;
e) Kutoa ushauri wa kisheria kwa Wabunge na uchambuzi wa miswada;
f) Kutoa huduma za Utafiti kwa Wabunge ("*Information Research*") pamoja na kukamilisha mfumo wa kidijitali wa Maktaba;
g) Kuratibu na kusimamia kazi na majukumu ya Tume ya Utumishi wa Bunge.
h) Kuwezesha Wabunge kushiriki kwenye baadhi ya Mikutano ya Kimataifa kama vile Mikutano ya Bunge la Afrika (PAP), Umoja wa Wabunge wa Jumuiya ya Madola (CPA) Kanda ya Afrika, CPA- International, Africa Caribbean Pacific and European Union (ACP/EU) na Jukwaa la Kibunge la Jumuiya ya Nchi za

Kusini mwa Afrika (SADC- PF), Bunge la Afrika Mashariki na Umoja wa Mabunge Duniani ( IPU);

i) Kuandaa vipindi vya televisheni na kurusha matangazo ya Bunge;

j) Kuratibu utoaji wa habari kwa wananchi kuhusu shughuli za Bunge na Kamati;

k) Kuratibu ushiriki wa Wabunge kwenye vikao vya Kamati na Bunge kwa kuwawezesha malipo ya posho na stahiki zao (Posho ya Jimbo, vikao, kujikimu na usafiri);

l) Kuratibu shughuli mbalimbali za kiutawala (huduma kwa Wabunge, ununuzi wa vifaa vya Ofisi, malipo ya maji, umeme na simu, usafi na ulinzi);

m) Kuwezesha matibabu ya Waheshimiwa Wabunge ndani na nje ya nchi;

n) Kuwezesha Watumishi kushiriki mafunzo ya muda mfupi na mrefu ndani na nje ya nchi;

o) Kuwajengea Wabunge uwezo ili waweze kutekeleza majukumu yao kikatiba;

p) Kusimamia uendeshaji wa Ukumbi wa Bunge, mitambo na mashine;

q) Kuratibu kazi ya kukarabati Jengo la ukumbi wa Bunge na majengo ya Ofisi ya Bunge pamoja na ujenzi wa nyumba ya Makazi ya Viongozi; na

r) Kugharamia maandalizi ya Bunge la Kumi na mbili (12).

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 5.1 Ofisi za Wabunge Majimboni

**Mheshimiwa Spika,** kamati bado inaendelea kusisitizia juu ya suala la ujenzi wa Ofisi za Wabunge majimboni na kuziwekea samani kwa utekelezaji wa majukumu yao kwa ufanisi pindi wanapokuwa majimboni. Aidha, Kamati inaona kuwa suala la ujenzi wa Ofisi za Wabunge ufanywe kupitia Mfuko wa Bunge na sio suala hili kukasimiwa kwa TAMISEMI;

### 5.2 Bima ya Afya kwa Wabunge baada ya ukomo wa Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** bima za afya zinazotolewa na NHIF kwa Waheshimiwa wabunge zinakoma tarehe 31 Juni, 2020 mara baada ya Bunge kuvunjwa. Hata hivyo, kwa Mujibu wa Katiba Ubunge hukoma pindi mbunge mwingine anapoteuliwa. Hivyo ni wazi kwamba lazima kuwe na utaratibu wa waheshimiwa wabunge kuwa na bima katika kipindi cha miezi minne kuanzia Juni hadi Oktoba 2020 pindi wabunge wapya watakapoapishwa. Hivyo, Kamati inaomba suala hili muhimu lichukuliwe kwa uzito wake na kufanyiwa kazi.

### 5.3 Kuboresha mfumo wa Bunge Mtandao *(e-Parliament)*.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapenda kukupongeza wewe binafsi na watendaji wa Ofisi ya Bunge kwa kusimamia na kuhakikisha Bunge linaanza kutumia mfumo wa Bunge Mtandao kwa lengo la

kuongeza ufanisi. Matunda ya matumizi ya Mfumo huu yameanza kuonekana na yameweza kusaidia katika kuendesha shughuli mbalimbali za Bunge hasa kwa kipindi hiki cha mripuko wa ugonjwa wa Corona. Aidha, Kamati inashauri Ofisi ya Bunge kuendelea kuboresha mfumo huu ili uweze kuongeza tija zaidi ikiwa pamoja na kuweza kutumika nje ya mipaka ya Bunge kwa kuzingatia usalama katika kupakia na kupakua nyaraka mbalimbali za Bunge na Serikali.

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** naomba nihitimishe kwa kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika na Naibu Spika kwa kuongoza vema mashauriano kati ya Kamati ya Bajeti na Serikali. Pia naomba kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango (Mb), Waziri wa Fedha na Mipango na Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Aidha, kipekee nimshukuru Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu) kwa kushirikiana na Kamati wakati wa majadiliano kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa maoni na mapendekezo mbalimbali kuhusu Bajeti ya Mfuko wa Bunge. Naomba kuwatambua wajumbe hao kama ifuatavyo;

1) Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb – M/Mwenyekiti
2) Mhe. David Ernest Silinde, Mb
3) Mhe. Mbaraka Kitwana Dau, Mb
4) Mhe. Mendrad Lutengano Kigola, Mb

5) Mhe. Maria Ndilla Kangoye, Mb

6) Mhe. Dkt. Immaculate Swale Semesi, Mb

7) Mhe. Ali Hassan Omar, Mb

8) Mhe. Freeman Aikael Mbowe, Mb

9) Mhe. Martha Jachi Umbulla, Mb

10) Mhe. Makame Kassim Makame, Mb

11) Mhe. Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mb

12) Mhe. Albert Obama Ntabaliba, Mb

13) Mhe. Oran Manase Njeza, Mb

14) Mhe. Riziki Said Lulida, Mb

15) Mhe. Hasna Sadi Katunda Mwilima, Mb

16) Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajabu, Mb

17) Mhe. Abdallah Majurah Bulembo, Mb

18) Mhe. Prof. Anna Kajumulo Tibaijuka, Mb

19) Mhe. Stephen Julius Masele, Mb

20) Mhe. Marwa Ryoba Chacha, Mb

21) Mhe. Balozi Diodorus Buberwa Kamala, Mb

22) Mhe. Joseph George Kakunda, Mb

23) Mhe. John Kibera Kishimba, Mb

24) Mhe. Andrew John Chenge, Mb

25) Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb

26) Mhe. Suleiman Ahmed Saddiq, Mb

27) Mhe. Dkt. Raphael Masunga Chegeni, Mb

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua fursa hii, kumshukuru Ndg. Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha, napenda kuipongeza na kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ikiongozwa na Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti Ndugu Michael Kadebe kwa kuratibu na kutoa ushauri wa kitaalamu ambao umesaidia Kamati katika kukamilisha taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Bunge – Fungu 42, kwa Mwaka wa Fedha 2020/21 kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**Mheshimiwa Spika,** naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Mashimba M. Ndaki, Mb
**M/MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI**

01 APRILI, 2020